

SOUTHERN TANZANIA ELEPHANT PROGRAM STEP

*Kulinda amani ya baadae kwa tembo wa kusini mwa Tanzania na kwingineko*

## Karibu kwenye jarida la STEP, robo ya kwanza Januari–Aprili 2016

**Southern Tanzania Elephant Program (STEP)** ni mradi wa uhifadhi wa tembo ulioko kusini mwa Tanzania. Tunafanya kazi na mamlaka za uhifadhi wa wanyamapori na jamii inayoishi maeneo ya hifadhi ili kuongeza ulinzi tembo na binadamu kuendelea kuishi na tembo kwa uvumilivu. Pia tunafanya utafiti husika za kisayansi za uhifadhi.

### Kusaidia askari wanyamapori wa Pori la Akiba la Rungwa

Tunayo fahari kusaidia askari wanyamapori wa Pori la Akiba la Rungwa kufanya doria na kuwatia nguvuni majangili wa tembo na mbao katika kitovu cha Pori la Akiba kwa wakati wa msimu wa mvua. STEP inatoa mafuta kwa ajili ya magari, mawasiliano na vifaa vya kuongoza njia, na kuendelea kusaidia doria kwa njia ya ndege – hii inasaidia wafanyakazi kugundua kambi za majangili wakiwa angani na kusaidia kupanga doria za nchi kavu. Timu ya askari wanyamapori wamerudisha katika hali nzuri kambi zilizopo mbali na makao makuu ya pori na zilizokuwa zimeachwa na kutawaliwa na majangili na kuongeza ulinzi katika kambi hizo. Mwaka huu, tumegawa chakula cha dharura mara mbili kwa kutumia ndege kwa askari wanyamapori waliokuwa wamekwama kutokana na mvua kubwa.

Ruaha-Rungwa ni sehemu muhimu sana kwa tembo, ambapo ujangili umeshamiri kwa miaka ya karibuni, na tunawapongeza askari wanyamapori wanaojitahidi kuhakikisha eneo hili linakuwa salama. Shukrani za dhati kwa Lady Amelie na African Wildlife Foundation, ambao wanatoa msaada binafsi kuiunga mkono kazi hii. Shukrani pia kwa David Moyer ambaye ni rubani, kwa kusaidia katika doria kwa njia ya ndege, na Peter Fox kwa kutoa msaada wa mkopo wa muda mfupi wa ndege ya Cessna 150.

Kwa wakati huu timu ya ndege ya STEP, Charles na Anne Nagy wanafanya kwa bidii maandalizi ya kuhamisha ndege yetu mpya kutoka Afrika Kusini. Hii ni baada ya ile ndege yetu, Skubie, kupata ajali mbaya mwezi November. Tunayo furaha kupata ufadhili kwa ajili ya ndege mpya, ambayo itaanza kazi ya ufuatiliaji wa tembo katika msimu ujao wa kiangazi.





STEP imekuwa ikitoa msaada wa doria kwa njia ya ndege katika msimu wa masika kwa askari wayamapori wa pori la Akiba la Rungwa.

## Mafunzo ya GPS na GIS kwa askari wanyamapori wa Rungwa

Matumizi ya teknolojia ya GIS (Geographical Information Systems) yamekuwa yana umuhimu mkubwa katika utekelezaji wa sheria kwenye maeneo mengi ya hifadhi. Ili kuongeza uwezo kwa ajili ya ufanisi katika matumizi ya teknolojia ya GIS katika Pori la Akiba la Rungwa, Kizigo na Muhesi, meneja wetu wa teknolojia ya uhifadhi, Frank Lihwa, alitoa mafunzo ya siku mbili kwa wafanyakazi 33 wa Pori la Akiba la Rungwa. Askari wanyamapori 24 walishiriki katika mafunzo ya GPS, wakijifunza jinsi ya kurekodi doria, kukusanya data, na kuongoza njia kwa kutumia GPS. Frank alifundisha askari wengine 9 namna ya kutengeneza ramani na kuchambua data za doria kwa kutumia QGIS, ambayo itasaidia idara ya ulinzi katika kuchanganua jitihada, matokeo na mipango ya utekelezaji wa sheria.




Frank Lihwa akitoa mafunzo ya GPS kwa askari wa Pori la Akiba la Rungwa kwa siku mbili.

## Mafunzo ya Kutembela Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wanafunzi wa sekondari ya Lundamatwe, Iringa

Mwezi March na Aprili, maafisa utafiti na uelimishaji kutoka STEP, Jenipha Mboya na Rehema John waliwafundisha wanafunzi katika shule ya sekondari Lundamatwe kuhusu viumbepori na uhifadhi nchini Tanzania, na kuandaa matembezi ya siku moja katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Magari mawili yalitumika kubeba wanafunzi 75 na walimu 10 katika safari kuelekea Ruaha, ambapo waliweza kuona mbuga ya Ruaha na viumbepori mbalimbali vilivyopo katika hifadhi hii. Wanafunzi walijifunza aina mbalimbali za uoto wa asili wa Ruaha, biolojia ya kuvutia na tabia za wanyama waliopo hifadhini. Pia Rehema aliweza kuwashirikisha wanafunzi kuhusu tafiti za tembo zinazofanywa na STEP, na aliwaelekeza namna ya kutofautisha kati ya tembo mmoja na mwingine kwa kutumia masikio na meno yake. Wanafunzi walifurahi kuwaona simba, tembo na mbuni, pia walifurahi kupata uzoefu wa kukwama kwenye matope katika msimu wa masika kwenye hifadhi. Programu hii ya kutembela hifadhi ya taifa ya Ruaha ilifanyika kwa ushrikiano mzuri na Lyra Africa, na tunapenda kumshukuru Maria Spink na Godfrey Kilawe kwa mpango na ushirikiano wao.




Wanafunzi kutoka shule ya sekondari ya Lundamatwe walitembelea hifadhi ya taifa ya Ruaha mwezi Apri

## Mradi mpya wa mshikamano baina ya binadamu na Tembo, Kilombero

Tunayo furaha kuanza kufanya kazi na wakulima katika miradi yetu wiwili mipya ya uzio wa mizinga ya nyuki iliyopo katika vijiji vya bonde la kilombero, ambavyo vimeathiriwa sana na tembo kutokana kuharibiwa mazao. Mwezi Aprili tulifanya mkutano na wanachama wa kikundi cha ufugaji nyuki cha Uadilifu kutoka kituo cha Msolwa (kilichopakana na pori la akiba la Selous) na wanakijiji wa kijiji cha Mkula (kilicho karibu na Hifadhi ya Taifa ya milima ya Udzungwa) kutambulisha mradi wa fensi za mizinga ya nyuki kama kizuizi cha uharibifu wa mazao unaofaywa na tembo, ikiwa ni pamoja na kujipatia faida ya kipato kutokana na mauzo ya asali. Wanachama wa kikundi cha wakulima cha Njokomoni ambao husimamia fensi ya mizinga ya nyuki iliyopo katika kijiji cha Mang'ula walifika pia katika mkutano ili kuelezea ujuzi na uzoefu wao katika huu mradi.

Watu wengi wana shauku juu ya huu mradi mpya wa mshikamano baina ya binadamu na tembo, na tumeanza hatua za kupanga mipango ya fensi za mizinga ya nyuki, ikiwa ni pamoja na kuagiza mizinga (Kwa sasa tunao ufadhili wa mizinga 40 kwa kila kijiji) na kufuatilia njia za tembo mashambani. Wakulima wataanza kujenga fensi wakishirikiana na wafanyakazi wa kujitolea kutoka katika kampuni ya Raleigh katika msimu ujao wa kiangazi.




Wanachama wa mradi mpya wa fensi za mizinga ya nyuki katika kituo cha Msolwa na Mkula.

## Ufuatiliaji wa tembo Ruaha: Msimu wa mvua na uzao mpya

Musimu huu wa mvua umesababisha changamoto katika miezi michache ya kazi za utafiti ndani ya Hifadhi ya Ruaha, na kwa sasa timu yetu ya utafiti wamekuwa wataalamu wa kuondoa magari yaliyonasa kwenye tope la udongo mweusi. Masaa yaliyotumia katika kukwamua magari yaliyonasa kwenye tope, yalikuwa ni muhimu katika data tulizo kusanya, kwa sababu tuliweza kurekodi data nyingi za tembo waliozaliwa miezi hii michache iliyopita, zilizo tupatia habari muhimu kuhusu kuzaliana kwa tembo. Tulifurahia pia wakati ambao tembo walijiingiza kwenye tope zuri na kuoga mbele yetu!



Landrover iliyo kwama kwenye tope



Tembo akifurahia kuoga kwenye tope

## Ajira mpya…

### Frank Lihwa – Meneja wa Teknolojia ya Uhifadhi



Frank amehitititimu shahada ya uzamili katika masomo ya Geographical Information Systems (GIS) katika chuo kikuu cha Aberdeen (Scotland), pia amefuzu shahada ya sayansi ya usimamizi wa mazingira katika chuo kikuu cha Ardhi (Tanzania) . Frank huongoza miradi ya STEP ihusianayo na technolojia ya uhifadhi, Ikiwa ni pamoja na kuchora ramani na uchambuzi wa data kwa kutumia teknolojia ya GIS na mfumo wa ufuatiliaji kwa njia ya ardhi.

### Kephania Mwaviko – Mfuatiliaji katika mradi wa muingiano baina ya binadamu na tembo

Kepha alijiunga nasi mnamo mwezi Desemba kufanya shughuli za ufuatiliaji wa muingiliano baina ya Tembo na binadamu katika mipaka ya hifadhi ya Taifa ya Ruaha iliyopo kusini mwa Tanzania. Kepha ni mwenyeji wa kijiji cha Makifu kilichopo jirani na Ruaha, pia amefuzu kama kiongozi wa utalii (Tour guide) katika chuo cha utalii cha Mkuyu kilichopo Tungamalenga. Kepha anatimiza ndoto zake za kufanya kazi na jamii kwa kutembelea zaidi ya vijiji 20 na kujifunza jinsi binadamu na tembo wanavyo ingiliana, pia hurekodi mapito na shoruba za tembo karibu na Ruaha.



## … na kwaheri



Mwezi huu tunasikitika kuagana na Rehema John, Afisa Utafiti na Uelimishaji, ambaye amekuwa pamoja nasi kuanzi Januari akishughurika na utafiti wa mshikamano baina ya binadamu na tembo, pia alihusika katika programu ya kuongoza wanafunzi kutembelea hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Tuna mtakia kila la kheri katika majukumu yake mapya kama Afisa wanyama pori katika idara ya wanyama pori Tunashukuru sana kwa mchango wake. Kwaheri Rehema!

## Habari kuhusu Tembo na Uhifadhi

- Mnamo mwezi machi, raia wawili wa kichina walihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela katika Mahakama ya hakimu mkazi Kisutu Dar es salaam kwa kosa la kuuwa tembo 226. Kesi hii ilichukua zaidi ya miaka miwili toka kukamatwa hadi kuhukumiwa, lakini ni faraja kuona matokeo (japo bado kuna nafasi ya kukata rufaa) ambayo yatakuwa kama kizuizi halisi kwa wafanya biashara wengine wa meno ya tembo waliopo nchini. Shukrani za dhati kwa waziri aliyepita Mh. Kagasheki na timu yake kwa kuwafikisha watuhumiwa, katika timu ya waendesha mashtaka na kwa hakimu Mkeha

- Pongezi kwa shirika la huduma za wanyamapori Kenya (Kenya Wildlife Service) ambalo mwishoni mwa mwezi April wameteketeza ghala lao lote la meno ya Tembo lililo salia. -lenye jumla ya tani 106- hii itatuma ujumbe kwa ulimwengu kwamba Tembo *wana umuhimu zaidi wakiwa hai*.Kampeni ya watanzania,*OKOA Tembo wa Tanzania* inafanya kampeni ili Tanzania kufanya hivyo pia, pia kampeni hii imeandaa barua ya wazi kwa Raisi John Magufuli kuomba kuteketezwa kwa ghala la meno ya Tembo-kubwa kuliko yote ulimwenguni.

- Mwezi Aprili, Meneja wa utafiti Josephine Smit na Mtafiti wa Tembo Lameck Mkuburo walirushwa katika Televisheni ya Taifa ya Tanzania wakifanya mahojiano na mwandishi wa habari Maggid Mjengwa wa *Nyumbani na Diaspora* katika kituo televisheni cha TBC1. Walijadili tabia na ikolojia ya Tembo, janga la ujangili na mshikamano baina ya binadamu na tembo, pamoja na kazi za STEP zifanyikazo kusini mwa Tanzania. Josephine pia alialikwa kama muongeaji mkuu katika kongangamano la Global Issues Service Summit, mkutano wa wanafunzi uliofanyika katika Shule ya Kimataifa ya Tanganyika Dar es Salaam mnamo mwezi Machi. Tazama hotuba yake kuhusiana na mazingira na jinsi vijana wanavyoweza kujihusisha nayo hapa.



Josephine akizungumza katika kongamano la wanafunzi Dar



Ndege mpya kwaajili ya programu ya doria

## Kusaidia STEP

STEP hutegemea ukarimu na wema wa wafadhili wetu. Tafadhari fikiria kutusaidia katika njia zifuatazo:

- **Changia katika programu yetu ya doria kwa njia ya ndege!** Tunauhitaji wa haraka wa fedha kwaajili ya kusaidia doria kwa njia ya ndege kwa askari wanyamapori katika pori la akiba la Rungwa. Ufadhili wa **$150** utasaidia kufanya doria ya anga dhidi ya ujangili kwa saa moja katika mazingira haya muhimu.
- Changia katika nyanja za kazi yetu kwa chaguo lako – Au katika OKOA Tembo wa Tanzania – kwa kututuma ujumbe kwa barua pepe kupitia info@stzelephants.org.
  - **TSH 70,000** ($30) hununua mzinga mmoja wa nyuki kwa ajili ya mradi wetu wa mshikamano baina ya binadamu na tembo
  - **$300** italipia kitengo kimoja cha GPS kwaajili ya askari wa Pori la akiba Rungwa
  - **$600** itanunua seti mpya ya taili kwa ajili ya gari moja kati ya ya magari yetu mawili ya yanayo tumika katika utafiti**.**
- Saidia wakulima wadogo wadogo na uhifadhi wa Tembo kwa kununua asali na kutembelea mradi wa fensi ya mizinga ya nyuki wa Njokomoni uliopo Udzungwa.
- Fuatilia STEP kwenye Facebook, Twitter, na kupitia Tovuti yetu, na shiriki katika kusambaza kazi zetu na habari zetu juu ya mambo yote yahusuyo tembo.

### Asante sana kwa msaada wako!

SOUTHERN TANZANIA ELEPHANT PROGRAM STEP

Registered not-for-profit No. 112972